**NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU**

**IDARA YA UANDISHI**

2 Machi 2013

Kwa Wabaha'i wa Irani,

Marafiki wapendwa sana,

Kwa muda wa miongo mitatu na nusu sasa, wimbi kufuatiwa na wimbi la mateso, yanayotofautiana kwa wakati yameikumba jumuiya yenu yenye kujaribiwa vikali na jasiri, mapigo ambayo ni ya karibuni kati ya yaliyomiminwa ndani ya miaka mia moja na sitini iliyopita. Bado, tofauti na matarajio ya wale wenye kujidhatiti kudhoofisha nguvu za jumuiya na wafuasi wa Baha'u'llah katika nchi alimozaliwa, hila zao, hatimaye zimesaidia kuimarisha misingi na kutia nguvu madaraja yake zaidi na zaidi ya raia wenu, ambao pia wao wakiwa wahanga wa udhalimu, sio tu kuwa wanaouona mtiririko wa uvunjifu wa haki ambao umesababishwa dhidi ya Wabaha'i katika miaka hiyo, bali pia utambuzi ndani ya viwango visivyozidiwa katika huduma yenye kutothaminiwa kwa jamii, nguvu ya mabadiliko ya kujenga. Kadiri ya huruma kwenu inavyoongezeka, ndivyo sauti za wito wa kuondolewa vikwazo ambavyo viliwazuia kutoshiriki katika maisha ya jamii katika mielekeo yote. Si cha kushangaza, basi, maswali yanayohusu mkao ulioshikiliwa na Wabaha'I kote kuhusiana na shughuli za siasa unachukua utambuzi mkubwa katika macho ya wazalendo wenzenu kihistoria, kwa kweli, nafasi ambamo jumuiya ya Kibaha'i ya Irani imejikuta katika heshima moja ya kipekee. Ilituhumiwa kimakosa, kwa upande mmoja, kwamba ilikuwa ya chimbuko la siasa ikisimamishwa dhidi ya utawala uliopo kuwa wakala wa nguvu ya kigeni ambayo mtuhumu alijidhihirisha kwa kusudi lake. Kwa upande mwingine kutokubali katu kwa watu wa jumuiya hii, kujiunga na shughuli za vyama vya siasa ambako kumeonekana kana kwamba ni kutojali mambo ya watu wa irani. Sasa kwa vile madhumuni ya kikweli ya wadhalimu wenu yamekuwa wazi, inawapasa ninyi kuitikia shauku inayokuwa ya wazalendo wenzenu kutaka kuelewa msimamo wa Wabaha'i kuhusiana na siasa, isije uelewa mbaya ukaruhusiwa kudhoofisha vifundo vya urafiki mnaojenga na mioyo mingi. Katika hili wanastahili matamshi machache, lau kama muhimu yale yanayoamsha sura ya upendo na umoja. Kuwasaidia katika kuwafikishia muono wa muundo ambao hujenga mbinu ya Kibaha'i katika suala hili, tunawapatieni matamko haya chini.

Kisichotenganishwa kutoka kwenye msimamo wa Kibaha'i katika siasa ni wazo mahususi la kihistoria, mtiririko wake na uelekeo. Ubinadamu, ni usadiki imara wa kila mfuasi wa Baha'u'llah, leo unakaribia hatua ya kufikia taji katika mchakato wa millenia nzima ulioleta kutoka kwenye uchanga wa pamoja ilimradi kufikia kwenye kizingiti cha ukomavu hatua ambayo itashuhudia kuleta umoja wa mbari ya binadamu. Pasipo tofauti ya mtu binafsi anayepita katika ujana usio na utulivu lakini wa kipindi cha barehe chenye matarajio, ambamo nguvu zilizofichika na uwezo hutokeza katika mwanga, binadamu wote pamoja wamo katikati ya mbadiliko usioweza kupimika. Nyuma ya msukosuko mwingi na sekeseke za maisha ya sasa kuna hila na viashiria vya ubinadamu unaokazana kufikia na ukomavu. Matendo na makongamano vinavyokubalika sasa, mienendo na tabia zinazoshangiliwa, moja baada ya nyingine zinaachwa kutumika, kwa jinsi mahitaji ya ukomavu yanaanza kujitokeza yenyewe.

Wabaha'i wanahimizwa kutazama mabadiliko ya mapinduzi yanayochukua nafasi ya kila anga za uhai kama jumuiko la michakato muhimu miwili. Mmoja ni mharibifu kiasili, wakati mwingine wa ujengefu; yote inashughulika kuubeba ubinadamu kila moja kwa jinsi yake, katika njia inayoelekea

kwenye ukomavu wake kamili. Utendaji wa ule wa awali ukionekana dhahiri kila mahali - katika mageuzi

ambayo yamezikumba asisi mahususi kongwe, katika unyonge wa viongozi katika ngazi zote kunusuru mipasuko inayotokeza katika maumbo ya jamii, katika hali ya kusambaratika kwa kawaida za jamii ambazo zilishikilia kwa muda mrefu uangalizi dhidi ya mataminio machafu na katika upotofu wa matumaini na kutojali vinavyooneshwa si watu binafsi tu bali pia jamii zote ambazo zimepoteza hisia hai za makusudio. Japo vinahuzunisha katika matokeo yake, nguvu za uvunjaji zinaelekeza kufagilia mbali vizuizi ambavyo huzuia maendeleo ya binadamu, na kufungua nafasi kwa ajili ya mchakato wa ujengaji ikivuta makundi mbalimbali pamoja na kufunua fursa mpya ya ushirikiano na Wabaha'i, kwa hakika, wao wanajitahidi kujipanga wenyewe, mmoja mmoja na kwa pamoja na zile nguvu zinazojihusisha na ujengaji, ambazo, wanahakika, zitaendelea kupata nguvu, hata kama kuna ukame katika upeo wa karibu. Mambo ya binadamu yatapangwa upya na amani ya ulimwengu itazinduliwa.
Huo ndio mwonekano wa historia inayoambatana na kila juhudi inafanywa na jumuiya ya Kibaha'i.

Kama mjuavyo kutokana na ujifunzaji wa maandiko matakatifu, kanuni ambayo itapenya kila kipengele cha maisha yaliyopangiliwa juu ya sayari ni umoja wa binadamu, kitambulisho cha umri wa ukomavu. Kwamba binadamu ni mkusanyiko wa watu wamoja ni ukweli ambao ukitizamwa kwa kujiuliza, unadai kukubalika kwa mapana leo. Kukataliwa kwa pandikizo la kina la chuki na hisia ya uzalendo wa ulimwengu inayokua ni kati ya ishara huu utambuzi unaokwezwa. Bado, hata kama matarajio ya kuongezeka kwa utambuzi wa pamoja uwepo, iangaliwe kama hatua ya mwanzo tu wa mchakato utakaochukua miongo kadhaa – la karne nyingi kufunuliwa. Kwa kanuni ya umoja wa binadamu, kama ilivyotangazwa na Baha'u'llah, haihitaji tu ushirikiano kati ya watu na mataifa. Inaitisha mawazo mapya ya kiushirikiano ya kudumisha jamii. Migongano ya kudidimia kwa mazingira, inayoendeshwa na muundo unaodekeza maangamizi ya mali ya asili kuridhisha kiu isiyopungua ya kudai zaidi, inapendekeza dhahiri kutotosheka kwa wazo la sasa la uhusiano uliopo wa binadamu na asili, uharibifu wa mahali pa makazi, vikisindikizwa na kupanda kwa unyonyaji wa kimpangilio wa wanawake na watoto duniani kote, vinaweka wazi jinsi isivyotakikana kuzaliwa kwa imani potofu ya kuyaelezea mahusiano ndani ya familia moja; na ung'ang'anizi wa utawala, kwa upande mmoja, na ongezeko la kupuuza mamlaka, kwa upande mwingine, vinatambulisha jinsi isivyotosheleza kwa binadamu wanaokomaa, kwa uhusiano wa sasa kati ya mtu binafsi na asasi za jamii, malimbikizo ya utajiri wa mali mikononi mwa wachache wa idadi kubwa ya dunia inatoa ishara ni vipi ambavyo kimsingi yamepotoka mawazo ya mahusiano kati ya sekta zilizo nyingi kwa kile ambacho sasa ni kutokeza kwa jumuiya ya ulimwengu. Kanuni ya umoja wa binadamu, kwa hivyo humaanisha basi, mabadiliko ya kimuumbo ndani ya muundo wenyewe wa jamii.

Kinachotakiwa kuelezewa wazi wazi hapa ni kwamba Wabaha'i hawaamini mabadiliko yaliyo kwenye muono hayatapatikana kipekee kupitia jitihada zao. Wala hawajaribu kuunda msukumo utakao tafuta kushinikiza juu ya jamii muono wao wa siku za usoni kwa jamii. Kila taifa na kila kikundi – kwa hakika, kila mtu binafsi – watatoa, kwa kiwango kikubwa au kidogo mchango kwa ustaarabu wa ulimwengu unaoinuka ambao kwao binadamu pasipo kizuizi wanaelekea. Umoja utapatikana kwa taratibu, kama ambavyo ilivyodokezwa awali, na 'Abdu'l-Baha, katika nyanja tofauti za maisha ya kijamii, mathalan, "umoja katika uwanja wa siasa", "umoja wa fikra katika shughuli za kidunia", "umoja wa kimbari", na "umoja wa mataifa". Vile haya yakiwa yanafikiwa, maumbo mengine ya dunia ya muunganiko wa kisiasa, ambayo yataheshimu utofauti mzima wa kitamaduni na kutoa mianya , utambulisho wa staha na heshima, vitapata sura pole pole.

Swali linalokuja kwa jumuiya ya ulimwengu wa Kibaha'i, basi ni vipi wataweza kuchangia vyema kwenye mchakato wa ujenzi wa ustaarabu kulingana na ukuaji wa rasilimali zao. Inaona miraba miwili ya uchangiaji wao. Wa kwanza ikihusiana na ukuaji na uendeleaji wake yenyewe, na ya pili kwa ushirikaji wake katika jamii pana.

Kuhusiana na ya kwanza, Wabaha'i duniani kote, katika mipangilio isiyo ya kusadikisha,

wanajibidiisha kuweka utaratibu wa shughuli sanjari na miundo ya kiutawala vinavyoibua kanuni ya umoja wa bianadamu na mambo yanayoisimika, machache yanayoelezewa hapa chini kama njia ya kielelezo: Kuwa roho timamu haina jinsia, mbari, kabila au tabaka, ukweli ambao haustahimili aina zote za ubaguzi, hata kwa uchache ule unaomzuia mwanamke kutimiza uwezo wake na kujiingiza katika nyanja tofauti za shughuli bega kwa bega na wanaume; kwamba mzizi wa chuki ni ujinga, ambayo yaweza kufutwa na michakato ya kielimu inayoweza kufikiwa na wanadamu wote, ikihakikishwa kuwa haitokei kumilikiwa na wenye fursa wachache; kwamba sayansi na dini ni miundo miwili yenye kushabihiana ya maarifa na vitendo ambavyo kwavyo binadamu hufikia kupata kufahamu dunia inayowazunguuka na kupitia kwake ustaarabu husonga mbele; kwamba dini bila sayansi ghafla hupukutikia katika ushirikina na ushabiki wa kidini; wakati sayansi bila dini hutokea kuwa chombo kichafu cha malidunia; kwamba ukwasi wa kweli, tunda la uwiano hai wa malidunia na mahitaji ya kiroho ya maisha, vitaendelea kufifia zaidi na zaidi visiweze kufikiwa, ikiwa ulaji utaendelea, utatumika kama bangi kwenye roho za binadamu; kama haki, ambayo ni kitivo cha roho, inawezesha mtu binafsi kubainisha ukweli kutokana na ulaghai na huongoza utafiti wa uhalisia, muhimu, ikiwa imani za kishirikina na desturi zilizopitwa na wakati zinazozuia umoja zipate kuondoshwa; kwamba itakapowekwa sawa sawa juu ya maswala ya kijamii, haki ndicho chombo pekee muhimu kwa kuuweka umoja; kwamba kazi inayofanywa na mtu kwa moyo wa huduma kwa wanadamu wenzake ni namna ya sala, njia ya kumwabudu Mungu. Kutafsiri njema kama hizi katika uhalisia, kusababisha mabadiliko kwenye ngazi ya binafsi na kuweka misingi ya miundo ya kijamii inayofaa, siyo kitu kidogo, kuwa na hakika, lakini jumuiya ya Kibaha'i imejiweka wakfu kwa mchakato wa muda mrefu wa ujifunzaji ambao kazi hii inajumuisha, mradi ambamo idadi iongezekayo kutoka nyanja zote za maisha, kutoka kila kundi la binadamu, wakaribishwa kushiriki.

Ni mengi, kwa hakika, maswali ambayo mchakato wa ujifunzaji, unaoendelea sasa katika sehemu zote za dunia, yajielekeze: Jinsi gani uwalete watu wanaotoka sehemu tofauti pamoja katika mazingira ambayo, yamejitenga na vitisho vya kila mara vya migongano na ikijtofautisha kwa mawenendo wake wa kiibada uwape hamasa ya kuweka kando njia zao za mivutano ya mwelekeo wa akili ya kimakundi, kuweka hali ya kiwango cha juu cha umoja wa fikra na vitendo, kuhamasisha kwa moyo wote ushiriki, namna ya kuhudumu maswala ya jumuiya ambamo hamna tabaka la utawala wenye nyadhifa za kidini ambao huweza kudai hadhi na fursa; namna ya kuwezesha safu za wake kwa waume kujiachia kutoka kwenye vifungo vya utepetevu na minyororo ya udhalimu ili kushiriki shughuli zenye kulingana na maendeleo yao ya kiroho, kijamii na kiakili; namna ya kusaidia vijana kuwa manahodha kupita hatua muhimu ya maisha yao na kuwezeshwa kuelekeza nguvu zao kuelekea uendelezaji wa ustaarabu; jinsi ya kuweka misisimko katika familia pekee yenye kuongoza katika kustawisha malidunia na kiroho bila kuwaingiza katika vizazi vinavyoinukia hisia za utengano wa dhana ya "wao" au kulea hulka ya kuwanyonya wale walioachwa kwa kundi hili, na kufanya uwezekano wa kufanyika maamuzi na kufaidika kutokana na utofauti wa mitazamo kupitia michakato ya ushauriano ambayo, ikieleweka kama utafiti wa hakika wa pamoja, unaohamasisha kujitenga kwa mtu binafsi kutoka hoja za binafsi, unaotoa umuhimu kwa taarifa za kimahesabu, usioibua tu hoja za jinsi hali ilivyo tu au kufafanua ukweli kuwa ni suluhisho kati ya makundi yenye uhasimu. Uchunguzi wa maswali kama haya na mengine mengi ambayo kwa hakika yatatokeza, jumuiya ya Kibaha'i imechukua namna ya utendaji inayochukua mwenendo wa kutenda, kutafakuri, kushauriana na kujifunza – kujifunza ambako huhusisha siyo tu urejeaji wa mara kwa mara kwenye maandiko matakatifu ya imani lakini pia kwenye upembuzi wa kisayansi wa mipangilio inyojitokeza. Kwa hakika, ni namna gani unadumisha mkao kama huo wa kujifunza ukitenda, ili kuhakikisha kwamba idadi inayoongezeka, washiriki katika kukuza na kutumia maarifa na jinsi ya kuweka miundo ya kufanya mpangilio kwa ajili ya uzoefu unaopanuka duniani kote na kwa ajili ya mgawanyo sawia wa mafunzo tuliyosoma - haya ndiyo, yenyewe, mambo ya uchambuzi wa mara kwa mara.

Mwelekeo mzima wa mchakato wa ujifunzaji ambao jumuiya ya Kibaha'i inaouchukua unaongozwa na mipango kadhaa ya kiulimwengu, ambayo nyenzo zake zimewekwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Ujengaji uwezo ndiyo angalizo la mipango hiyo: zinaelekezwa katika kuwezeshwa watenda kazi wa juhudi ya pamoja ya kuimarishwa misingi ya kiroho ya vijiji na ujirani, kushughulikia mahitaji kadhaa ya kijamii na kiuchumi, na kuchangia katika mijadala inayoendelea katika jamii, na yote wakiendelea kudumisha mshikamano muhimu katika mbinu na namna.

Kwenye moyo wa mchakato wa ujifunzaji ni swali la asili ya mahusiano ambayo umefunga mtu binafsi, jamii - watendaji ambao kwenye jukwaa la historia walifungwa katika mapambano ya tawala wakati wote. Katika hali hii, dhana ya kuwa mahusiano kati yao kwa vyovyote yataambatana na shuruti za ushindani, wazo ambalo hupuuza uwezo mkubwa wa roho ya binadamu, umewekewa pembeni kupisha sehemu ambayo kwamba suluhu ya mjumuiko wao waweza kukuza ustaarabu ufaao jamii komavu. Kuhusisha juhudi ya Kibaha'i kugundua asili ya mahusiano ya washiriki hao watatu ni muono wa jamii ya siku za usoni ambayo inapata uvuvio kutoka kwenye uchambuzi uliotolewa na Baha'u'llah, katika waraka ulioandikwa yapata karne na nusu iliyopita, ambayo hulinganisha dunia na mwili wa mwanadamu. Ushirikiano ni kanuni ambayo huongoza utendaji wa muundo huo. Kama ambavyo kujitokeza kwa roho pekee katika huu uwanja wa kuwa umewezeshwa kupitia mwingiliano mgumu wa chembe chembe zisizohesabika, ambazo mpangilio wake katika minofu na viungo hutoa fursa ya kupatikana kwa uwezo mahususi, hivyo ustaarabu uweze kuonekana kama matokeo ya mafungu ya mwingiliano wa karibu sana kati ya viungo vilivyotofauti na vyema kufumwa pamoja, ambavyo vimeuepuka kwa ufinyu kusudi la uwepo wao wenyewe. Na kama uhitaji wa uwepo wa kila chembe chembe na kila kiungo ni tegemezi kwa afya. Kiwiliwili chote, ndivyo hivyo ustawi wa kila mmoja, kila familia, kila watu utafutwe katika hali njema ya mbari nzima ya wanadamu. Kuegemea muono huo, asasi, kwa kuthamini utendaji wenye kuratibiwa kuelekea mwisho wenye matunda mengi, hazilengi kuthibiti bali kulea na kuongoza mtu binafsi, ambaye naye kwa upande wake hupokea miongozo kwa ukunjufu siyo katika utii wa ukipofu, bali kwa imani katika msingi wa ufahamu hai. Ndani ya jamii, wakati huo, huchukuliwa changamoto ya kuhakikisha hali ya kudumisha ambamo nguvu za watu binafsi, ambao hupenda kuonyesha uwezo wao wa kujieleza kiwajibu kulingana na kawaida na pia katika mipango ya asasi, ikiongezeka ndani ya juhudi ya pamoja.

Iwapo utando wa mahusiano ulioelezewa hapo juu ukipata sura na kuinua mfumo wa maisha wenye kutofautishwa na kushikilia kwake kwenye kanuni ya umoja wa binadamu, misingi kadhaa ya kimtazamo italazimika kupimwa kwa uangalifu. Yenye kutanabaishwa sana ni mtazamo wa madaraka kwa uwazi mtazamo wa madaraka kama nyenzo ya kutawala, ikisindikizwa na mawazo ya kiushindani, mashindano, migawanyiko na, kujikweza, ni lazima viachwe nyuma. Hii siyo kukataa kuwapo kwa madaraka; awali ya yote, hata katika mambo ya asasi za kijamii, zilipata mamlaka kupitia ridhaa ya watu, madaraka yanahusika katika kuendesha mamlaka. Lakini michakato ya kisiasa, kama michakato mingine ya kimaisha, haiwezi kubakia pasipo kuguswa na tawala/mamlaka zingine za kiroho za binadamu ambazo imani ya Kibaha'i - - kwa hali hii, kila desturi ya dini zote kuu iliyowahi kutokea katika nyakati zote hutegemea kuchota: nguvu ya umoja, ya upendo, ya huduma nyenyekevu, ya matendo safi. Kwa kushirikishwa na madaraka katika hali hii kuna maneno kama "achilia" "hamasisha", "pitishia", "ongoza" na "wezesha". Mamlaka si upekee kamili ambao waweza 'kutwaliwa' na kulindwa "kiwivu"; Yanajumuishwa na uwezo usio na kipimo chenye uwezo wa kufanya mabadiliko katika kila kinachoishi ndani ya mbari ya binadamu kama mwili.

Jumuiya ya Kibaha'i hukubali kwa haraka kuwa ina kiasi fulani cha umbali wa safari kabla ya uzoefu wao unaokua kuzalisha umaizi muhimu ndani ya utendaji vifungu vinavyohitajika vya muingiliano. Haifanyi madai ya ukamilifu. Kushikilia juu maadili na kufikia utimilizo, vyake si kitu kimoja na siyo kile kile – changamoto ni nyingi mno zilizoko mbele, na mengi bado yanahitaji kujifunza.

Mchunguzi wa kawaida aweza tu kuona kama jaribio la jamii hii kutundika changamoto hizi "kimawazo". Lakini kwa hakika haiwezi kuwa haki kuonyesha Wabaha'i kama wasiojali maswala ya nchi zao, licha ya kutokuwa wazalendo. Hata kama ni kimawazo vipi, juhudi za Wabaha'i zaweza kuoneakana kwa wengine, duku duku zao za kina za maslahi ya binadamu haziwezi kupuuzwa. Na kufuatia ukweli kuwa hakuna mpango sasa hivi duniani wenye kuonesha uwezo wa kuinua binadamu kutoka katika tinga tinga la ufarakano na mapingano, na kunusuru utulivu wake, ni kwa nini serikali yoyote yaweza kupinga juhudi za kundi moja la watu kujizamisha katika kutaka kufahamu asili ya yale mahusiano muhimu yenye taswira moja kwa wote katika siku za usoni ambako mbari ya binadamu inakokotwa kiujumla? Kuna ubaya gani katika hili?

Katika mfumo uliokwisha nakiliwa kutokana na mawazo yaliyokwisha tajwa hapo juu, basi, kuna uwezekano wa kufikiria kipimo cha pili cha juhudi za jamii ya Wabaha'i kuchangia uendelezaji wa ustaarabu: Kujishughulisha kwake ndani ya jamii yote. Kiuwazi kila wanachokiona Wabaha'i kama moja ya mlengo wa kuchangia kwao hakuwezi kukinzana na mwingine. Hawawezi kuwa wanatafuta kuweka mifumo ya kiakili na vitendo vinavyotoa ufafanuzi wa kanuni ya umoja ndani ya jumiya yao, bado washiriki katika shughuli za mtizamo tofauti ambao kwa kipimo chochote, unaimarisha vifungu ambavyo vinalenga dhana tofauti kabisa juu ya uwepo wa kijamii. Kuepuka uwili kama huo, jumuiya ya Kibaha'i imeendelea kusafisha wakati wote, kwenye misingi ya mafundisho ya imani, mambo makuu ya ushiriki wao katika maisha ya jamii. Ya kwanza na ya mbele kabisa, Wabaha'i hujibidiisha, ikiwa ni watu binafsi au kama jumuiya, kuweka katika vitendo amri za Baha'u'llah: "Wale ambao wamejaliwa na ukweli na uaminifu lazima wahusiane na watu wote na vizazi vya dunia kwa shangwe na wangavu, kwa jinsi kwamba kuongea na watu kumekuza na kutaendelea kukuza umoja na uhusiano ambavyo kwa upande wake huweka hali njema kwa ajili ya kutunza utulivu katika dunia na kwa kukuza mataifa". Ni kupitia "ushirikiano na kukutana," Abdu'l-Baha ameeleza zaidi, kwamba "tunapata furaha na maendeleo, binafsi na kwa pamoja" "kile ambacho hukubalika katika ushirikiano na mvuto na umoja kati ya wana wa watu," Ameandika kuhusiana na hili, "ni njia ya maisha ya ulimwengu wa binadamu." Hata katika suala la dini, Ameweka wazi wazi kuwa "ni lazima iwe kichocheo cha upendo na maelewano. Ikiwa dini itatokea kuwa chanzo cha mabishano na uadui, kutokuwepo kwake ni bora." Hivyo ndivyo ilivyo Wabaha'i hufanya kila lililo katika uwezo wao wakati wote kutimiza ushauri wa Baha'u'llah, "fumba macho yako kwa utengano, kisha kodolea juu ya umoja." Huyo mmoja hakika ndiye mtu", Huwaasa wafuasi wake, "ambaye, ni leo, hujitoa kwa ajili ya huduma kwa umati mkubwa wa binadamu". "Muwe macho kwa mahitaji ya wakati mnamoishi," ni onyo kutoka kwake, "na elekeza mazungumzo yenu kwenye maagizo na mahitaji." "Hitaji kuu kabisa la binadamu ni ushirikiano na uelewano, "Abdu'l-Baha alielekeza. "wa udugu na mshikamano kati ya binadamu, ndivyo nguvu zaidi za ujengaji zinakua zaidi na mafanikio yote katika nyanja zote za shughuli za binadamu." "Ni wenye nguvu kubwa mno mwangaza wa umoja" Baha'u'llah atangaza, "kwamba waweza kuangazia dunia nzima".

Ni kwa kuwa na mawazo kama haya moyoni kwamba Wabaha'i huingia katika ushirikiano kadiri ambavyo rasimali zao huwaruhusu, ndani ya uongezekaji wa harakati; asasi, makundi na watu binafsi, wakiweka ubia wenye kukazana kuleta mabadiliko ya jamii na kusongesha hoja ya umoja, kukuza ustawi wa jamii, na kuchangia mshikamano wa dunia. Hakika, viwango vinavyowekwa na maelezo ya hapo juu huchagiza jamii ya Wabaha'i kujihusisha kwa uhai katika nyanja nyingi za maisha ya kawaida iwezekanavyo. Katika kuchagua maeneo ya ushirikiano, Wabaha'i waweke akilini kanuni, ambazo zimekitwa ndani ya mafundisho, ikiwa na maana wawe na mwendelezo kuelekea mwisho, malengo mema hayawezi kupatikana kwa kutumia njia zisizofaa. Hasa hasa, haiwezekani kujenga umoja wa kudumu kupitia juhudi zinazohitaji mabishano au kufikiria kuwa muendelezo wa tofauti za kimaslahi ndiyo msingi wa mwingiliano wa binadamu, hata ikiwa ya kukomoa. Hapa iangaliwe kwamba, pamoja

na mapungufu yanayo wekwa na kushirikiana kwenye kanuni hii, jumuiya haijapata kuuona upungufu wa fursa za ushirikiano, hivyo watu wengi dunani leo wanafanya kazi kwa umakini sana kuelekea lengo moja au lingine ambalo Wabaha'i hushiriki. Katika mkutadha huu, huchukua hadhari ili wasije vuka mipaka fulani na wenzao na washirika. Hawatochukulia ushirikiano wowote kama nafasi ya kuwaburuza wengine katika masuala ya kiimani. Kujikweza na mambo ambayo kwa bahati mbaya hujitokeza kama ukereketwa wa kidini unapaswa kuepukwa kabisa. Wabaha'i, hata hivyo, huwapatia washirika wao mafunzo waliokwisha yapata kupitia uzoefu wao, kama ambavyo hufurahia kuunganisha katika jitihada zao za ujenzi wa jumuiya umaizi uliopatikana kutokana na ushirikiano kama huo.

Hii inatufikisha, hatimaye, kwenye swali mahususi la shughuli ya kisiasa. Imani ya jumuiya ya kibaha'i kwamba jamii ya binadamu ikiwa imepita hatua za mwanzoni za mageuzi ya kijamii, sasa ipo kwenye kizingiti cha ukomavu wa binadamu wa pamoja; Imani yake kuwa kanuni ya umoja wa binadamu, kituo cha rika ya ukomavu, huashiria mabadiliko katika muundo mzima wa kijamii; kujitolea kwake katika mchakato wa ujifunzaji, kwamba kwa kuchangizwa na kanuni hii, huchambua ufanyaji kazi wa vifungu vya ushirikiano kati ya mtu binafsi, jumuiya na asasi za kijamii, washriki watatu katika uendelezaji wa ustaarabu; imani yake kwamba upitio mpya wa madaraka, ukiwa huru kutokana na fikra ya ukandamizaji pamoja na kusindikizwa na mawazo ya mapambano, ushindani, migawanyiko na kujikweza, huweka kigezo kinachohitajika cha vifungu vya ushirikiano; kujidhatiti kwake kwenye muono wa ulimwengu kwamba, manufaa yatokanayo na utajiri wa tamaduni tofauti za binadamu, haikubali njia zozote za migawanyiko - haya yote hukusanya vipengele vya mfumo ambao huunda mbinu ya Kibaha'i kwenye mambo ya siasa kama inavyoelezewa kwa ufupi hapa chini:

Wabaha'i hawatafuti madaraka ya kisiasa. Hawatakubali vyeo vya kisiasa katika serikali zao, kwa mpangilio wowote uliopo, japokuwa watakubali vyeo ambavyo wataviona ni vya kiutawala tu kiasili. Hawatajiambatanisha na vyama vyovyote vya kisiasa, kukwepa kunaswa na mambo ya vyama vya siasa, au kushiriki katika programu zenye agenda za kugawa katika kundi lolote au kujitenga. Wakati huo huo, Wabaha'i huheshimu yoyote ambaye, kutokana na hamu ya moyo safi kutaka kutoa huduma kwa nchi zao, huchagua kuingia katika ulingo wa kisiasa au kujishughulisha na siasa. Mbinu iliyochukuliwa na jamii ya Kibaha'i ya kutojihusisha na shughuli hizi haikusudiwi kama tambo lenye kumaanisha msimamo mkali unaokataza siasa katika ukweli wake kimantiki; kwa kweli, binadamu hujipanga wenyewe kupitia shughuli zao za kisiasa. Wabaha'i hupiga kura katika uchaguzi wa kiraia, mradi wasijitambulishe kuambatana na chama cha siasa chochote ili kufanya hivyo. Katika muktadha huu, huiona serikali kama mfumo wa kudumisha ustawi na utaratibu wa jamii, na wao hufanya, mmoja na wote hutii sheria za nchi ambamo huishi, bila kuruhusu itikadi yao ya kidini ya ndani kuvunjwa. Wabaha'i hawatokubali uchochezi wowote wa kupindua serikali. Wala hawaingilii mahusiano yoyote ya kisiasa kati ya serikali tofauti za mataifa tofauti. Hii haimaanishi kuwa wao ni wajinga katika michakato ya kisiasa ya dunia ya leo, na kwamba hawatofautishi kati ya serikali ya haki na ya utawala wa udhalimu. Watawala wa dunia wanawajibu mtakatifu wa kutimiza kwa watu wao, ambao wanapaswa kuangaliwa kama hazina ya thamani kubwa ya taifa lolote. Popote wanakoishi, Wabaha'i hujibidiisha kushikilia viwango vya haki, wakiangalia uonevu unaoelekezwa kwao au kwa wengine, ila kupitia njia za kisheria zilizopo mbele yao, Wakijitenga na aina zozote za migomo ya vurugu. Zaidi ya hapo, hakuna kinachoweza kubadili mapenzi waliyonayo ndani ya mioyo yao kwa ajili ya binadamu katika hisia zao kwenye wajibu wanaotarajia kuutimiza kwa nguvu zao katika huduma kwa nchi zao husika.

Mbinu au mkakati, endapo, pamoja na vifungu rahisi vya ziada vilivoelezewa katika aya iliyotangulia vinawezesha jumuiya, katika dunia ambamo mataifa na makabila hukinzana moja dhidi ya mwenzake na watu wamegawanyika na kutengwa na miundo ya kijamii, kudumisha mshikamano wao na heshima kama mtandao mmoja na kuhakikisha kuwa shughuli za wabaha'i katika nchi moja hazihatarishi za wale walioko kwingineko. Wakijihadhari na mashindano ya maslahi ya mataifa na

vyama vya siasa, jumuiya ya Kibaha'i, basi ndipo inaweza kujenga uwezo wake kuchangia katika mchakato ambao unakuza amani na umoja.

Marafiki wapendwa: Tunatambua kwamba kutembea katika njia hii, ambavyo mmefanya kwa uwezo mkubwa kwa miongo kadhaa, haikosi kuwa na changamoto. Inadai hadhi ambayo haiwezi kutikiswa, kwa unyoofu wa tabia usioweza kughilibiwa, kwa uelewa wa wazi wa fikra usioweza kutiwa giza, kwa upendo mtu kwa nchi yake usioweza kuchezewa. Sasa kwa vile wananchi wenzenu wanapoelewa masaibu yenu na kinachowezekana watajifungua kwenu bila shaka ili muweze kushiriki zaidi na zaidi katika maisha ya jamii, tunasali ili muweze kupewa msaada kutoka katika kuelezea kwa marafiki zenu na wazalendo wenzenu muundo ulioambatanishwa katika kurasa hizi ili kwamba, kwa ushirikiano nao, mtapata nyongeza ya fursa kufanya kazi kwa faida ya watu wenu bila kusalimisha, kwa namna yoyote utambulisho wenu kama wafuasi wa Mmoja Ambaye aliita binadamu, zaidi ya karne moja iliyopta, kwenye Utaratibu Mpya wa Ulimwengu.

**Imesainiwa na: Nyumba ya Haki ya Ulimwengu**